**TANGAZO LA SERIKALI Na. …………………….. la Tarehe ………………………..**
**SHERIA ZA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA, 1982**

---

**SURA YA 290**

---

**SHERIA NDOGO**

---

**Zimetungwa chini ya vifungu vya 7(2) na 16(1)**

# SHERIA NDOGO ZA ADA NA USHURU ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA BUTIAMA ZA MWAKA, 2025.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina

1. Sheria Ndogo hizi ziitwe Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Butiama za Mwaka 2025 na zitaanza kutumika mara baada ya Kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Butiama.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo, tafsiri za maneno zitatumika kama ifuatavyo:-

Sura ya 290

‘‘Sheria’’ maana yake ni Sheria za Fedha za Serikali za Mitaa;

’’Kiroba cha Mawe’’ maana yake ni kiroba chenye mawe ya dhahabu

‘‘Afisa Muidhiniwa’’ maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeidhiniwa kutekeleza chochote chini ya Sheria Ndogo hizi;

“Ada’’maana yake ni malipo yanayotozwa na Halmashauri kwa mtu yeyote anayeomba kibali ama ridhaa ya Halmashauri ya kufanya shughuli yeyote ambayo kwa mujibu wa sheria ndogo hizi inastahili kulipiwa ada

“ushuru” maana yake ni ushuru wa mazao ya mifugo au kilimo au misitu au bidhaa nyingine zinazotozwa chini ya sheria ndogo hizi;

Bidhaa, maana yake ni kitu chochote kinachouzwa sokoni gulioni, mnadani dukani au sehemu nyingine yeyote iliyoruhusiwa

‘‘Halmashauri’’ maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Butiama;

’’Mwalo ’’ maana yake ni eneo la kuoshea dhahabu baada ya mawe ya dhahabu kusagwa.

’’Plant ’’ Maana yake ni kinu cha kuozeshea dhahabu.

Huduma maana yake ni shuguhuli zote zinatotolewa na Halmashauri au mtu mwingine yeyote ambazo zinapaswa

kulipiwa ada kwa mujibu wa sheria ndogo.

‘‘Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri na itajumuisha Kaimu Mkurugenzi;

’’Soko’’ Maana yake ni sehemu au eneo maalum lililotengwa kwa ajili ya shughuli za kuuza na kununua bidhaa na mazao.

“Madini pemba” ni udongo maalum kwa ajili ya kutengeneza pemba unaopatikana katika mamlaka ya Halmashauri.

“Madini Ujenzi” maana yake ni pamoja na mchanga, kokoto, changarawe ,mawe, kifusi na malisili zingine za namna hiyo ambazo kwa kawaida hutumiwa kwa ujenzi katika eneo la Halmshauri.

“Lori la Mizigo” maana yake ni gari lolote lenye uzito kuanzia tani 4.5 ambalo hufanya kazi za kubeba mizigo ikiwa ni pamoja na madini ujenzi katika eneo la Halmashauri

‘‘Mwenyekiti’ maana yake ni Mwenyekiti wa Halmashauri;

Mazao mchanganyiko maana yake ni mazao yote yatokanayo na shughuli za kilimo,

“Mlipa ushuru’’ maana yake ni mtu yeyote anayehusika na ununuzi wa Ushuru wa Mazao ya Mifugo yanayozalishwa katika eneo la Mamlaka ya Halmashauri;

“Mnunuzi” maana yake ni mtu binafsi taasisi au kikundi cha watu kinachojishughulisha na ununuzi wa mazao au mifugo

“Mnada” maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuuzia au kununulia mifugo.

“Ushuru wa huduma” maana yake ni malipo anayotoa mtu au mfanyabiashara kutokana na huduma anazozitoa kama iliyotafsiri katika sheria fedha ya serikali za mitaa.

“Mawasilisho” maana yake ni mawasilisho yote ya ushuru, nyaraka au maelezo yoyote yanayohitajika kuwasilishwa Halmashauri ambayo yanayofanywa na mlipa ushuru kuhusiana na kiasi cha Ushuru wa Mazao ya Mifugo kilichonunuliwa;

“Ushuru wa Mawe ya dhahabu” ni ushuru unatozwa katika maeneo ya uchimbaji wa dhahabu ambao wachimbaji hawana uwezo wa kuchakata dhahabu mpaka mwisho.

“Muuzaji” maana yake ni mtu binafsi, taasisi au kikundi cha watu kinachojishughulisha na uuzaji wa bidhaa, mazao au mifugo.

“Waziri” maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa:

“Ushuru” maana yake ni fedha zote ambazo Halmashauri itatoza kwa mazao na mifugo iliyouzwa katika masoko magulio minada na machinjio ni fedha zote ambazo Halmashauri inatoza kwa mujibu wa sheria ndogo hizi.

“Ukumbi” maana yake ni sehemu iliyoandaliwa kwa ajili ya sughuli za mikutano au shughuli nyingine zinazofanana na hizo.

“Mwaka wa fedha” maana yake ni Mwaka wa Fedha kama unavyotambuliwa Serikali;

“Mazao ya Mifugo” maana yake ni mazao yoyote

yanayotokana na mifugo inayofugwa au inayopatikana ziwani, na mtoni kama vile ng'ombe, mbuzi, kondoo, na wanaofanana nao na samaki,vigugu, dagaa na aina zote za samaki wanaopatikana katika eneo la Mamlaka ya Halmashauri:

"Kibali cha sherehe" maana yake ni idhini ya kufanya sherehe anayopewa mkazi aliyepokatika mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Butiama.

## SEHEMU YA PILI
## JINSI YA KUTOZA/ KUKUSANYA USHURU

Malipo ya Ada/Ushuru

4. (1) Halmashauri itatoza ushuru na ada kutokana na huduma au bidhaa zinazotolewa kwa malipo katika eneo lake huduma hizo zikijumuisha utoaji wa vibali ,ushuru wa mazao ya mifugo ,mazao mchanganyiko,mazao ya misitu, madini ujenzi madini pemba madini ya dhahabu, lesseni mbalimbali na nyinginezo kama inavyoonyesha katika jedwali ya sheria ndogo hizi.

(2) Ada na ushuru unaotozwa chini ya sheria ndogo hizi utalipwa kabla ya kutolewa kwa huduma husika au vinginevyo kama itakavyoamriwa na kuelekezwa na Mkurugenzi kwa maandishi

Wajibu wa kulipa Ada/ushuru

5. (2) Mtu yeyote anayewajibika kulipa ada na ushuru atalipa ada au ushuru huo kabla ya kupata huduma au kutoa huduma husika au vinginevyo kama itakavyoamriwa na kuelekezwa na Mkurugenzi kwa maandishi;

(3) Malipo ya ushuru yataambatana na taarifa za mawasilisho zinazobainisha kiasi cha Ushuru wa kila huduma aliyopata ama kiasi kilichokusanywa na Mhusika kwa minaajili ya kufanya hesabu kamili za malipo ya ushuru aliyoikusanyia Halmashauri.

Ushuru wa maegesho ya malori ya mizigo

6. (1) Halmashauri itatoza ushuru wa maegesho kwa malori yote ya mizigo yanayofanya kazi katika eneo lake;

(2) Kila mmiliki wa lori la mizigo atawajibka kulipia na kupewa kibali kinachoruhusu lori lake kufanya kazi katika eneo la Halmashauri.

(3) Ushuru wa kibali cha lori la kusafirisha mizigo utalipwa kama unavyotajwa katika jedwali la sheria ndogo hizi.

(4) Malipo ya ushuru unaotozwa kwa mujibu wa sheria ndogo hizi utalipwa kwa Halmashauri au wakala wake ambaye atatoa stakabadhi ya malipo kama kielelezo cha malipo;

(5) Ni wajibu wa mlipa ushuru yeyote kudai na kuhakikisha anapewa stakabadhi halali kwa malipo anayotoa.

Ushuru wa stendi

7. (1) Halmashauri itatoza ushuru kwa magari yote yanayoingia katika stendi kuu ya mabasi kwa namna na kiasi kilichotajwa katika jedwali la sheria ndogo hizi.

(2) Halmashauri katika utozaji wa ushuru kwenye mabasi yanayoingia stendi vitatofautiana kulingana na ukubwa basi hivyo basi kwa mabasi madogo na makubwa yatatozwa

viwango tofauti kama inavyoonyesha kwenye jedwali la sheria ndogo hizi

(3) Halmashauri itatoza ushuru kwa kila mtu anayeingia stendi kupata huduma ya kusafiri kuchukuwa mizigo au kuingia stendi kwa shughuli zake binafsi isipokuwa wamiliki wa sehemu za kufanya biashara na wasafiri wenye tiketi hawatatozwa ushuru .Aidha ushuru huu utatozwa kama inavyoonyeshwa kwenye majedwali ya sheria ndogo hizi.

(4) Halmashauri itatoza ushuru wa magari ya watu binafsi wanaoingia stendi kupata huduma mbalimbali au kupeleka abiria wanaosafiri isipokuwa kwa wamiliki wa sehemu za kufanya biashara hawatozwa ushuru.

Ushuru wa mazao mchanganyiko

8. (1) Halmashauri katika maeneo yake ya utawala itatoza ushuru wa mazao mchanganyiko ambao ni mahindi mtama ulezi mpunga maharage alizeti karanga,viazi, udaga dengu, na mazao mengine yatakayolimwa kwenye eneo la Halmashauri kwa kiwango kilichoanishwa kwenye jedwali chini ya sheria ndogo hizi.

(2) Halmashauri itatoza ushuru wa mazao ya biashara ambayo ni katani, pamba kahawa na mengineyo yenye mrengo wa kibiashara kwa miongozo inayotolewa na Wizara.

Ushuru wa mazao ya Bustani

9. (1) Halmashauri itatoza mazao ya bustani yanayolimwa ndani ya Halmashauri ya Butiama kwa kuzingatia viwango vilivyoanishwa kwenye jedwali la sheria.

Kibali cha kusafirisha mazao

9(1) (a) Halmashauri itatoza kibali cha kusafirisha mazao kwa mfanyabiashara aliyenunua mazao katika mamlaka ya Halmashauri kwa kiwango kilichoanishwa kwenye jedwali za sheria ndogo hizi

(b) Kwamba kibali hicho kitatolewa kabla ya mfanyabiashara kutoa mazao yake katika eneo la kiutawala la Halmashauri.

Skimu za umwagiliaji

10. (1) Halmashauri itaanzisha skimu za umwagiliaji katika mamlaka yake ya utawala ili kurahisha shughuli za kilimo na umwagiliaji.

(2) Halmashauri itatoza Kibali cha umwagiliaji kwa wakulima watakaokuwa wanatumia skimu za umwagiliaji katika mamlaka yake ya utawala kwa kiwango kilichoanishwa kwenye jedwali la sheria ndogo hizi.

Kwamba Halmashauri itatoza ada ya utunzaji wa skimu ya umwagiliaji kwa wakulima wanatumia skimu za umwagiliaji zilizopo katika Halmashauri.

## SEHEMU YA NNE
## USHURU WA MADINI UJENZI NA DHAHABU

Ushuru wa Madini Ujenzi

11. (1) Halmashauri itatoza ushuru wa madini ujenzi ambao utajumuisha mchanga ,kokoto, kifusi cha udongo, mawe yanayopatikana katika Vijiji au maeneo yanayomilikiwa na Halmashauri yenyewe.

(2) Kwamba Halmashauri itatoza ushuru wa madini ujenzi kwa mita qubiki hivyo mmiliki wa lori atatakiwa kulipa ushuru wake kuendana na ujazo wa lori kama ilivyoanishwa kwenye jedwali la sheria ndogo hizi.

(3) Kwa wamiliki wa viwanda vya kuchakata kokoto watawajibika kulipa kodi ya ushuru wa huduma kwa Halmashauri kama inavyooelekeza sheria ya fedha ya serikali za mitaa sura ya 290.

Ushuru wa kiroba cha mawe ya dhahabu

12. (1) Halmashauri itatoza ushuru wa kiroba cha mawe ya dhahabu kwa wachimbaji ambao mfumo wa uendeshaji na uchakataji wa dhahabu ni ule wa rashi na mmiliki hachakati dhahabu hadi mwisho.

(2) Halmashauri itatoza ushuru wa kiroba kwa wachimbaji wadogo wote wenye leseni ya uchimbaji madini lakini hawana uwezo wa kuchakata dhahabu hadi mwisho.

Ushuru wa makinikia

13. (1) Halmashauri itatoza ushuru wa makinikia kwa wachimbaji wa madini wa aina zote yaani mchimbaji mdogo wa kati na mchimbaji mkubwa pale ambapo kampuni itaamua kusafirisha makinikia kutoka katika eneo la uzalishaji.

(2) Halmashauri itatoza ushuru wa makinikia katika mauzo yote yatakayofanyika kati mchimbaji au mmiliki wa kifusi kilichouzwa kwa ajili ya kuozesha ambapo tozo hizo zitakuwa kama zilivyanishwa kwenye jedwali la sheria ndogo hizi.

(3) Kwamba Halmashauri itatoza tozo ya makinikia kwa mnunuzi anayesafirisha kutoka nje ya wilaya ya Butiama ushuru wa makinikia.

Ushuru wa karasha

14. (1) Kwamba kila mmiliki wa lesseni ndogo ya uchimbaji wa madini ya dhahabu ambao wanatumia mfumo wa rashi katika shughuli za uchimbaji watatakiwa kulipa ushuru wa Karasha kwa mwezi.

(2) Kwamba ushuru huu unaweza kulipwa na mmiliki wa lesseni mwenyewe mpangaji au mtu yeyote anayefanya shughuli za kusaga mawe ya dhahabu katika eneo la mmiliki wa lesseni ya uchimbaji.

(3) Kwamba ushuru wa karasha utalipwa kwa mwezi na mmiliki wa lesseni au mfanyabiashara anayefanya kazi ya kusaga mawe katika eneo la mmiliki wa lesseni.

Ushuru wa madini pemba

15. (1) Halmashauri itakusanya ushuru wa madini pemba katika maeneo yanayozalisha madini pemba.

(2) Kwamba ushuru huu utatozwa kwa kwa mnunuzi wa madini pemba kabla hajasafirisha kutoka katika eneo la uzalishaji.

(3) Kwamba ushuru huu utatozwa kwa kila kiroba kilichozalishwa kwa kuzingatia viwango vilivyoanishwa kwenye jedwali la sheria ndogo hizi.

Ushuru wa karasha

16. (1) Halmashari itatoza ushuru wa karasha kwa wachimbaji wadogo au mmiliki wa lesseni ya msingi ambao wanaendesha lesseni hiyo kwa mfumo wa rashi.

(2) Kwamba mmiliki yeyote wa karasha atatakiwa kulipa ushuru wa karasha hizo zinazofanya biashara na wachimbaji wadogo ambao husaga mawe ya katika eneo lenye lesseni ya msingi.

(3) Kwamba ushuru wa karasha utatozwa kwa mmiliki wa karasha kila mwezi ambapo atatakiwa kulipa ushuru wa tsh 15,000 kama inavyoonekana katika jedwali la sheria ndogo hizi.

Ushuru wa mwalo

17. (1) Kwamba Halmashauri itatoza ushuru kwa mmiliki wa mwalo aliye katika lesseni ya uchimbaji mdogo au asiye katika eneo lenye lesseni ya uchimbaji mdogo.

(2) Kwamba ushuru wa mwalo utotozwa kwa mialo inayofanya kazi isipokuwa pale mwalo unaposimama au unapofungwa mmiliki anatakiwa kutoa taarifa kwa Mkurugenzi Mtendaji kuhusu kufungwa kwa mwalo huo.

(3) Kwamba wakati Halmashauri inakusanya ushuru wa mwalo pia watakagua vitendea kazi kwa watumishi walioajiriwa na mmiliki wa mwalo lengo ni kulinda afya za watumishi katika mialo ambapo zoezi litaendeshwa na afisa mazingira wa Wilaya.

(4) Kwamba ushuru wa mwalo utalipwa kwa mwezi kwa kuzingatia viwango vilivyoanishwa katika jedwali la sheria ndogo hizi.

Ushuru wa plant

18. (1) Kwamba kila mmiliki wa mitambo ya kuozesha dhahabu katika maeneo ya Halmashauri anatakiwa kulipa ushuru kwa Halmashauri kutokana na shughuli zake za kuozesha dhahabu.

2. Kwamba ushuru wa kuozesha dhahabu utalipwa kwa mwaka hivyo mfanyabiashara kabla ya kuanza kazi ya kuozesha anatakiwa kulipa ushuru huu kama ilivyoanishwa kwenye sheria ndogo hizi.

3. Kwamba ushuru wa kuozesha dhahabu utalipwa kwa kuzingatia viwango vilivyoanishwa katika jedwali la sheria ndogo hizi.

Ubebaji wa Madini ujenzi kwa kutumia bajaji

19. (a) Kwamba iwapo mmiliki ataamu kubeba madini ujenzi kwa kutumia bajaji za mizigo mmiliki wa bajaji atatakiwa kulipa ushuru wa Halmashauri.

(b) Kwamba mmiliki wa bajaji atalipa ushuru wa madini ujenzi kwa tripu na hivyo mkusanyaji anatakiwa kutoa risiti inayothibitisha malipo haya kwa kila trip.

(c) Kwamba kwa mimliki wa Bajaji au dereva wa bajaji ya mizigo atalazimika kulipa ushuru kwa trip na siyo kulingana na ujazo wa Bajaji yake.

## SEHEMU YA TANO
## USHURU WA MATANGAZO YA BIASHARA KWA NJIA YA SAUTI NA KUUZA BIDHAA KWENYE GARI

Ushuru wa Matangazo kwa njia ya sauti

20. (1) Halmashauri itatoza mtu yeyote anayetangaza biashara kwa kutumia gari zenye spika ambazo zinatoa matangazo kuhusiana na biashara yake kwa kuzingatia viwango vilivyoanishwa katika jedwali za sheria ndogo hizi.

(2) Kwamba kwa kila mtangazaji wa biashara yake anatakiwa kulipa ushuru wa matangazo iwapo anakusudia kutangaza matangazo ya biashara katika maeneo ya Halmashauri.

(3) Kwamba ushuru huu utalipwa kwa siku atakazotumia kutangaza matangazo katika maeneo ya Halmashauri na endapo atashindwa kulipa ushuru hataruhisiwa kutangaza katika eneo la Halmashauri.

Ushuru wa mobile shopo

21. (1) Kwamba mtu yeyote atakayefanya biashara katika eneo lisilo rasmi kwa kutumia miundo inayohamishaka kama gari au kontena ambalo lipo eneo wazi la Halmashauri, au maeneo yaliyoandaliwa kwa ajili ya gulio au mnada au matumizi mengine mtu huyo atakiwa kulipa ushuru kwa Halmasauri ya Butiama.

(2) Halmashauri itatoza ushuru huu kwa kuangalia siku ambazo mfanyabiashara ameweka kontena katika eneo wazi la Halmashauri au mnada kwa kuzingatia viwango vilivyoanishwa kwenye jedwali la sheria ndogo hizi.

(3) Kwamba ushuru huu utalipwa kabla ya mfanya biashara hajaanza kutumia eneo husika kwa ajili ya biashara ambapo itakuwa ni siku moja kabla ya kupanga bidhaa zake.

(3) Kwamba iwapo mfanyabiashara anafanyia biashara katika eneo la mnada atatakiwa kulipa ushuru huu siku hiyo kabla ya kupanga bidhaa.

Tozo ya kumbi za Halmashauri

22. (a) Kwamba Halmashauri itotoza ushuru wa kumbi zilizopo katika majengo kwa ajili ya kufanya shughuli za mikutano au shughuli za nyingine ambazo hazitaathiri ufanyikaji wa shughuli za Halmashauri.

(b) Kwamba kwa taasisi inayotumia ukumbi ambayo itashirikisha wataalum wa Halmashauri watalipa gharama za uendeshaji ambazo ni usafi , maji ,umeme na uchakavu wa miundo mbinu.

(c) Kwamba taasisi ambazo hazitatumia wataalum wa Halmashauri zitatakiwa kulipa tozo zilizoanishwa katika jedwali la sheria ndogo.

(d) Kwamba tozo za kutumia ukumbi wa Halmashauri zitalipwa kabla ya kuanza shughuli za kutumia ukumbi na endapo atashindwa kulipa kabla ya kuanza kutumia ukumbi atatakiwa kupata kibali kutoka Mkurugenzi Mtendaji (W) kinachoruhusu kuendelea shughuli hiyo.

Tozo ya vyombo vya matangazo

22. 1(a) Halmashauri itakodisha vyombo vyake vya matangazo kwa wananchi watakao hitaji kuvitumia vyombo hivyo kwa shughuli za matangazo.

22. 2(b) Kwamba Halmashauri itatoza ushuru wa kukodisha vyombo vya matangazo vinamilikiwa na Halmashauri kama ulivyoanishwa jedwali la sheria ndogo hizi.

## SEHEMU YA SITA
## ADA ZA HUDUMA ZA MACHINJIO NA UKAGUZI WA NYAMA

Ukaguzi wa Nyama

23. (1) Halamshauri itatoza ushuru wa ukaguzi wa nyama kwa mifugo yote iliyochinjwa katika maeneo yake kiutawala kwa kuzingatia viwango vilivyoanishwa katika jedwali la sheria ndogo hizi.

(2) Kwamba ushuru wa ukaguzi utalipwa kwa mtaalum wa mifugo ambaye amekasimiwa mamlaka ya kufanya ukaguzi wa nyama na afisa mifugo wa Wilaya ambapo atalipwa mara baada ya kufanya ukaguzi.

(3) Kwamba ushuru wa ukaguzi wa nyama utalipwa kwa kila mnyama atakayechinjwa na kukaguliwa na afisa aliyeidhishwa kukagua nyama.

Ushuru wa kulaza mifugo machinjio

24. (1) Halmashauri itatoza ushuru wa kulaza mifugo machinjio kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa awali kabla ya mifugo hiyo kuchinjwa.

(2) Kwamba ushuru utatozwa kwa mfugaji kabla hajaingiza mifugo husika katika zizi la serikali ambapo atalazimika kulipa ushuru kama ulivyoanishwa katika jedwali la sheria ndogo hizo.

Lesini ya mwamba

25. (1) Halmashauri itatoza leseni kwa wamiliki wa mwamba walioko katika maeneo ya Halmashauri ambapo itajumuisha watu binafsi na serikali za vijiji zinazomiliki mwamba.

(2) Kwamba ushuru wa mwamba utatozwa na Halmashauri kwa kuzingatia viwango vilivyoanishwa katika jedwali la sheria ndogo hizi.

Ushuru wa machinjio

26. (1) Kwamba Halmashauri katika maeneo yake itajenga machinjio yatakayomilikiwa na Halmashauri ambapo itatoza ushuru wa machinjio kwa kila mmanyama atakayechinjwa katika machinjio hayo.

(2) Halmashauri itatoza ushuru huu kabla ya mmiliki wa mfugo kumchinja kwa kuzingatia viwango vilivyoanishwa katika jedwali la sheria ndogo.

Ushuru wa mazao ya mifugo

27\. (1) Halmshauri itatoza ushuru wa mazao ya mifugo kwa wachuhuzi wanaofanya biashara ngozi, maziwa katika Wilaya ya Butiama.

(2) Kwamba ushuru wa mazao ya mifugo utatozwa kwa asilimia kama ilivyoanishwa katika jedwali la sheria ndogo hizi.

(3) Kwamba itakuwa ni kosa kwa mfanyabiashara ya bucha kuchinja nje ya machinjio au kuuza nyama nje ya bucha na endapo atafikishwa mahakamani na akakutwa na hatia atatozwa faini iliyoanishwa katika sheria ndogo hizi.

(4) Kwamba viwanda vinavyojishughulisha na uzindikaji wa maziwa vitatakiwa kulipa ushuru wa huduma kwa Halmashauri isipokuwa mfugaji au mlanguzi wa maziwa anatakiwa kulipa ushuru uliaoanishwa kwenye sheria ndogo hizi.

## SEHEMU YA NANE
## ADA YA KUSOMA NYARAKA ZA HALMASHAURI

Ada ya usomaji wa nyaraka

28\. (1) Halmashauri itatenga chumba maalum kwa ajili ya usomaji wa nyaraka za wazi ambazo Halmashauri imekasimiwa mamlaka ya kutunza na kulinda nyaraka hizo.

(2) Kwamba msomaji wa nyaraka za Halmasauri hataruhusiwa kurudufisha au kuzalisha nyaraka za Halmashauri bila kupata idhini kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji.

(3 Kwamba idhini ya kuzalisha nyaraka za Halmashauri itatolewa na Mkurugenzi Mtendaji mwenyewe au kaimu hivyo kabla ya msomaji kutoa kurudufisha nyaraka lazima apate kibali hicho.

(4) Kwamba kabla ya msomaji kusoma nyaraka atatakiwa kulipa ada ya usomaji wa nyaraka kwa afisa aliyekasimiwa mamlaka ya kukusanya ada hiyo kama ilivyoanishwa kwenye jedwali la sheria ndogo hizi.

(5) Kwamba iwapo mtu hasomi nyaraka za Halmashauri isipokuwa anatumia maktaba ya Halmasauri atatakiwa kulipa ushuru ulianishwa katika jedwali la sheria ndogo hizi.

(6) Kwamba iwapo msomaji atasoma Nyaraka lakini pia ana nia ya kuzalisha au kurudufisha atatakiwa kulipia kibali cha kurudufisha nyaraka hizo kama ilivyoanishwa katika jedwali la sheria ndogo .

## SEHEMU YA TISA
## SHUGHULI ZA UTAMADUNI

Kibali cha sherehe

29. (1) Kwamba kwa kila mwananchi anakusidia kufanya sherhe ya aina yeyote anatakiwa kulipia kibali cha kufanya sherehe hiyo kwa kuzingatia kiwango kilichoanishwa katika jedwali lililopo katika sheria ndogo hizi.

(2) Kwamba kibali cha sherehe kitatolewa na afisa utamuduni au afisa yeyote wa Halmashauri aliyeruhusiwa na Mkurugenzi Mtendaji kutoa kibali hicho kabla ya sherehe kuanza.

(3) Kwamba mara baada ya mwanchi kukabidhiwa kibali cha kufanya sherehe atatakiwa kuomba idhini katika kituo cha polisi ili aweze kupewa idhini ya kufanya mkusanyiko huo

Katazo

30. Itakuwa ni kosa kwa mwanachi yeyote kufanya sherehe ya aina yeyote pasipo kupata kibali cha kufanya sherehe kutoka Halmashauri na endapo atafanya sherehe bila kibali atahesabika ametenda kosa katika sheria ndogo hizi na akipatika na hatia atatozwa faini iliyoanishwa katika sheria ndogo hizi.

Kuendesha utafiti wa masuala ya kale

31. (a) Kwa mtu yeyote mwenye nia ya kufanya utafiti wa masuala ya kale katika eneo la Halmashuri atakiwa kulipia ada za kufanya utafiti huo kabla ya kuanza shughuli hiyo

(b) Kwamba iwapo anayefanya utafiti huo ni mgeni au siyo raia wa Tanzania atakiwa kulipa ada za kufanya utafiti huo kwa dola na iwapo ni raia wa Tanzania atatakiwa kulipa ada hiyo kwa fedha za Kitanzania kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali la sheria ndogo hizi.

Wauzaji wa dawa za Kienyeji

31 1(a) Kwamba kila muuzaji wa dawa za asili katika mnada au gulio anatakiwa kulipa ushuru kwa Halmashauri kwa kila siku ya gulio au mnadani.

2(b) Kwamba ushuru huu utalipwa kabla ya muuzaji kuanza biashara kwa afisa aliyekasimiwa mamlaka ya kutoza ushuru au wakala wa Halmashauri kwa kuzingatia viwango vilivyoanishwa katika jedwali la sheria ndogo hizi.

## SEHEMU YA TISA
## USHURU WA MAZAO YA MISITU

Ushuru wa mazao ya misitu

32. (1) Halmashauri itotaza ushuru wa mkaa kwa wauzaji wa mkaa wanaofanya shughuli zao katika eneo la utawala la Halmashauri ya Butiama.

(2) Kwamba shughuli za utozaji wa ushuru wa mazao ya misitu zitafanywa na Halmashauri kwa kushurikiana na Wakala wa misitu TSF ambao wako ndani ya Halmashauri Isipokuwa pale Halmashauri itatoa kibali au itatoza ushuru wa mazao ya misitu kwa muuzaji au mfanyabiashara, wakala wa misitu hawanatakiwa kutowatoza tena wafanyabiashara hao kwani wameshalipa kodi hivyo basi pale wakala wa misitu wanapokuwa wametoza ushuru wa mazao ya misitu Halmashauri haitakiwi kuwatoza tena wafanyabiashara hao vivyo hivyo pale ambapo Halmashauri itatoza wakala wa misitu hawatakiwi kutoza tena

(3) Kwa misitu inayomilikiwa na Halmashauri yenyewe wajibu wa kuvuna na kusimamia toza zinatozwa kwenye mazao ya misitu zitasimamiwa na Halmashauri yenyewe vivyo hivyo kwa misitu inayomilikiwa na wakala wa misitu yaani TSF wajibu wa kuvuna na kusimamia toza hizo itakuwa ni jukumu la wakala wa misitu waliopo katika Halmashauri

(4) Kwamba watu binafsi wanaomiliki misitu iliyopo katika maeneo ya utawala ya Halmashauri watakiwa kulipia kibali cha uvunaji kabla hawajaanza zoezi la uvunaji.

(5) Kwamba jukumu la kusimamia misitu ya watu binafsi litakuwa ni jukumu la Halmashauri yenyewe kwa kushiriana na mtaalam wa mazingira wa Halmashauri.

(5) Kwa mtu yeyote anayekusudia kuvuna miti yake lazima kupata kibali cha uvunaji kutoka kwa afisa mazingira ambapo kibali hicho kitalipiwa ushuru uliyoanishwa katika jedwali la sheria ndogo hizi.

(6) Kwamba ushuru wa mazao ya misitu utatoza na Halmashauri au wakala au afisa aliyekasimiwa mamlaka ya kutoza ushuru kwa kuzingatia viwango vilivyoanishwa kwenye jedwali la sheria ndogo hizi.

Ushuru wa Mirunda

33. (1) Halmashauri itotoza ushuru wa mirunda kwa mmiliki wa msitu au mtu yeyote anayekusudia kuvuna mirunda iliyopandwa katika eneo lake.

(2) Kwamba iwapo mmiliki wa msitu au mmiliki wa eneo lililopandwa miti anakusudia kuvuna mirunda atatakiwa kutoa taarifa kwa afisa maliasili ili aweze kumtoza ushuru huo.

(3) Kwamba ushuru wa mirunda utatozwa kwa kuzingatia viwango vilivyoanishwa katika jedwali sheria ndogo hizi.

Ushuru wa Magogo

34. (a) Kwamba mtu yeyote mwenye nia ya kusafirisha magogo ndani na nje ya Halmashauri atatakiwa kulipa ushuru kwa kila gogo analokusudia kusafirisha.

(b) Kwamba iwapo msafirishaji amevuna katika shamba atatakiwa kutimiza masharti yaliyoanishwa katika kifungu 32(5) cha sheria ndogo hizi.

(c) Kwamba ushuru wa magogo utalipwa kwa kuzingatia bei iliyoanishwa kwenye jedwali la sheria ndogo hizi.

## SEHEMU YA KUMI
## USHURU WA BIASHARA SOKONI

Ushuru wa biashara ndogo Mnadani/sokoni

35. (1) Halmashauri itatoza ushuru wa biashara ndogo ndogo zinazofanyika katika minada masoko na magulio yaliopo katika maeneo yake ya kiutawala.

(2) Kwamba ushuru huu utatozwa kabla mfanyabiashara hajaanza kupanga biashara yake na endapo atashindwa kulipa kabla hataruhusiwa kupanga biashara yake kwa siku husika.

(3) Kwamba ushuru huu wa biashara ndogo ndogo mnadani sokoni au gulioni zitatozwa kwa kuzingatia viwango vilivyoanishwa katika jedwali za sheria ndogo hizi.

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA
## USHURU WA MAEGESHO KATIKA MAENEO YA HALMASHAURI

Ushuru wa Maegesho

36. (1) Halmashauri itatoza ushuru wa maegesho kwa wamiliki wa vyombo vya usafiri watakaoegesha vyombo vyao katika maeneo ya utawala ya Halmashauri.

(2) Kwamba ushuru huu utatozwa kwa mmiliki yeyote aliegesha chombo cha usafiri katika maeneo ya utawala ya Halmashauri kama ilivyoanishwa kwenye jedwali la sheria ndogo hizi.

## SEHEMU YA KUMI NA MBILI
## ADA YA KUlAZA MAGARI NA MITAMBO ISIYO YA SERIKALI

Ushuru wa kulaza gari katika yadi ya Halmashari

37. (1) Halmashauri itatoza ushuru wa kulaza magari katika yadi zinazomilikiwa na Halmashauri ambapo mmiliki wake atakiwa kulipa ushuru kabla ya kulaza gari yake**.**

(2) Kwamba ushuru wa kulaza magari katika maeneo ya Halmashauri utatozwa kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa kwenye jedwali la sheria ndogo hizi.

## SEHEMU YA KUMI NA TATU
## USHURU WA HUDUMA

Ushuru wa huduma

38. (1) Halmashauri itatoza ushuru wa huduma kwa mujibu wa sheria ya fedha ya serikali za mitaa sura 290 kama ilivyofanyiwa marejeo 2020 kwa wafanyabiashara wote wanaofanyabiashara zao katika Halmashauri isipokuwa kuwa kwa mabenki .

(2) Kwamba kwa kampuni za uzalishaji wa madini zinatakiwa kulipa ushuru wa huduma kwa kila uzalishaji unapofanyika kwa kiwango cha asilimia 0.3 na endapo atachelewasha atalipa riba ya asilimia 4 ya ushuru aliotakiwa kulipa wakati wa uzalishaji.

(3) Kwamba wauzaji wa maduka reja reja na jumla watakiwa kulipa ushuru wa huduma wakati wa kulipa lesseni za biashara kwa kiwango cha asilimia 0.3.

(4) Kwamba iwapo mlipaji ataomba kupunguziwa ni sharti kuomba kupunguziwa asilimia kwa Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri na endapo ataridhia kupunguza basi atamjibu mlipaji kwa barua ambayo itaonyesha kiasi ambacho anatakiwa kusamehewa na anachotakiwa kulipa.

## SEHEMU YA KUMI NA NNE
## USHURU WA MALIWATO

Ushuru wa maliwato

39 (1) Halmashauri katika maeneo yake ya kutolea huduma za kijamii ikiwa ni pamoja na masoko mnada stendi na maeneo mengine ambayo Halmashauri itaona inafaa kutengeneza

miundo mbinu ya maliwato itatengeneza isipokuwa jamii itachangia gharama za uendeshaji.

(2) Kwamba Halmashauri itatoza ushuru wa maliwato kwa kuzingatia viwango vilivyoanishwa katika jedwali la sheria ndogo hizi hata hivyo ushuru huo utalipwa kabla ya mtumiaji kupata huduma**.**

(3) Kwamba itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote atakayeacha kutumia miundo mbinu ya maliwato na kujisaidia maeneo mengine ambayo hayana miundo mbinu husika na endapo atakamatwa atalipa faini papo kwa papo kwa kuzingatia viwango vilivyoanishwa kwenye jedwali la sheria ndogo hizi.

(4) Kwamba endapo mtu yeyote aliyekiuka kifungu cha 33(3) na akakataa kulipa faini aliyoambiwa atafikishwa mahakamani na akikutwa na Hatia atahukumiwa kifungo cha miezi kumi mbili jela pamoja na kulipa faini iliyoanishwa kwenye jedwali sheria ndogo hizi.

## SEHEMU YA KUMI NA TANO
## USHURU WA SAMAKI

Ushuru wa samaki

40. Halmashauri itatoza ushuru wa samaki wanaovuliwa kwenye ziwa, mito, na mabwawa kwa kiwango kinachobainishwa kwenye jedwali la sheria ndogo hizi.

Wakala

41. (1) Ushuru wa mazao ya ziwani utatozwa kwa wanunuzi wa samaki, vigugu, kambale au dagaa na aina zote za samaki wakati wa mnada.

(2) Wakala au afisa wa Halmashauri atakayeteuliwa na Halmashauri kutekeleza jukumu lolote chini ya Sheria Ndogo hizi, atawajibika kusimamia ukusanyaji huo kwa viwango vilivyoainishwa na Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hizi na kamwe hataruhusiwa kutoza viwango tofauti na vilivyobainishwa chini ya Sheria Ndogo hii.

(3) Mtu yeyote atakayeteuliwa kama wakala chini ya Sheria Ndogo hii, atakuwa na majukumu ya kukusanya ushuru na kumshitaki mtu yeyote atakayeshindwa kwa makusudi kulipa ushuru unaotakiwa kulipwa kwa wakala au mkusanyaji huyo kwa muda unaotakiwa katika Mahakama yenye Mamlaka ya kusikiliza shauri hilo kama madai katika kipindi cha muda wa mkataba wake na Halmashauri.

(4) Wakala ,afisa wa Halmashauri, kibarua, atakuwa na majukumu kwa Halmashauri kama ifuatavyo:-

(a) Kukusanya na kupokea ushuru kwa kiwango kilichoainishwa katika Sheria Ndogo hizi kwa niaba ya Halmashauri katika eneo ambalo ameteuliwa kukusanya ushuru husika;

(b) Kuwasilisha makusanyo yote aliyowajibika kukusanya kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala;

(c) Kumchukulia hatua za kisheria mtu yeyote ambaye atakiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi;

Uwezo wa kumuita mlipa ushuru

42. Mkurugenzi anaweza kumuita mlipa ushuru yeyote afike mbele yake au mbele ya Afisa muidhiniwa kwa muda unaofaa na kutoa maelezo yanayohitajika kuhusiana na malipo ya ushuru.

Uwezo wa Mkurugenzi kufifilisha kosa

43. Mkurugenzi anaweza kufifilisha kosa kwa kumtoza mlipa ushuru aliyetenda kosa, chini ya Sheria Ndogo hizi ikiwa mlipa ushuru huyo amekiri kwa maandishi kwa Mkurugenzi, kuwa ametenda kosa hilo na kuwa atalipa ushuru anaodaiwa pamoja na faini na kisha atapatiwa stakabadhi ya malipo hayo.

Uwezo wa Mkurugenzi Mtendaji

44. (1) Kwamba Mkurugenzi Mtendaji anaweza kupunguza kiasi cha ushuru kiliachoanishwa kwenye sheria ndogo hizi na kuruhusu kiasi pungufu kilipwe na mlipaji au kisilipwe kutokana na sababu atakazoziona yeye zinafaa baada ya kuashauriana na Mwenyekiti wa Halmashauri.

Kufungua Shauri Mahakamani

45. Bila ya kuathiri Sheria Ndogo ya 42 ,43 Sheria Ndogo ya 44, endapo mlipa ushuru yeyote atashindwa kulipa ushuru au adhabu, Halmashauri itafungua shauri la madai kwa njia ya mkato [summary procedure] katika Mahakama yenye uwezo wa kusikiliza shauri hilo.

Hati ya Kukamata Mali

46 (1) Bila ya kuathiri Sheria ndogo ya 45Halmashauri itakuwa na uwezo wa kisheria kuomba katika Mahakama yenye Mamlaka katika eneo la Halmashauri kukamata maliza mdaiwa wa ushuru wa Halmashauri aliyekiuka sheria ndogo hizi kwa kukataa kulipa ushuru anaodaiwa.

(2) Hati atakayopewa mlipa ushuru na Mahakama itakuwa na mamlaka ya kisheria ya kukamata na kuuza mali inayoondosheka ya Mlipa ushuru na kila hati ya madai ambayo itapelekwa Mahakamani kwa nia ambayo imeelezwa katika Sheria Ndogo hizi, itakuwa ni uthibitisho kamili wa maelezo ya madai yaliyoelezwa chini ya hati hiyo.

## SEHEMU YA KUMI NA SITA
## MAKOSA, ADHABU NA JINSI YA KUCHUKUA HATUA ZA KISHERIA

Deni

47. (1) Ushuru au na faini yoyote ambayo Halmashauri inadai kwa mtu yoyote, kikundi cha watu, Kampuni au Taasisi chini ya Sheria Ndogo hizi itakuwa ni deni la Halmashauri na litalipwa kutoka kwa mtu yeyote, kikundi cha watu, kampuni au Taasisi kupitia kwa Mkurugenzi au Afisa yeyote aliyeidhinishwa chini ya Sheria Ndogo hizi kwa niaba ya Mkurugenzi.

(2) Bila ya kuathiri maelezo ya jumla ya Sheria Ndogo ya 47 hapo juu, kuhusiana na jinsi ya kudai deni lolote la Halmashauri, ikiwa Afisa yeyote aliyeidhiniwa na Mkurugenzi atafungua shauri katika Mahakama yenye Mamlaka ya kusikiliza shauri na ataandaa hati ya malalamiko ambayo itaeleza uzito wa kosa na maombi kutokana na hati ya madai ya deni la Halmashauri pamoja na faida 20% ya deni hilo iliyoandaliwa dhidi ya mdaiwa yeyote kupelekwa Mahakamani..

(4) Kila hati ya madai ambayo itapelekwa Mahakamani kwa njia ambayo imeelezwa katika Sheria Ndogo hii, itakuwa ni uthibitisho kamili wa madai yaliyoelezwa katika hati hiyo.

Mdaiwa anaposhindwa kulipa deni

48. Ikiwa mdaiwa yeyote atatozwa faini chini ya Sheria Ndogo hizi na akashindwa kulipa deni hilo kwa wakati, Mahakama itaendelea kusikiliza shauri hilo kama kawaida inavyosikiliza mashauri mengine na itatumia mamlaka yake ama iongeze adhabu au itoe adhabu ya kifungo kwa mdaiwa yeyote kwa muda usiopungua miaka miwili au vyote kwa pamoja faini na kifungo.

Kukusanya ushuru bila Ruhusa

49. Mtu yeyote ambaye-

(a) Hajaruhusiwa na Halmashauri kwa maadishi kukusanya ushuru unayokusanywa chini ya Sheria Ndogo hizi;

(b) Amekusanya au amejaribu kukusanya ushuru kwa kiwango ambacho hakijatajwa chini ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa chini ya sheria Ndogo hizi na akithibitika kutenda kosa hilo atapewa adhabu iliyoanishwa katika Sheria Ndogo hizi;

Sheria Na. 49/ 1966

50. Bila ya kuathiri maelezo ya jumla ya Sheria Ndogo hizi, katika kudai deni la ushuru, Halmashauri itatumia Sheria ya Kanuni za Mwenendo wa Madai [Civil Procedure Code Act] na Halmashauri pia itapata faida kutokana na kiasi kinachotolewa na Benki kwa wakati husika.

Makosa

51. Mtu yeyote ikiwa ni mlipa ushuru, wakala au mkusanya ushuru ambaye:-

(a) Ameshindwa, amedharau, au amekaidi kulipa ushuru wa Mazao ya Mifugo chini ya Sheria Ndogo hizi;

(b) Ameshindwa, amedharau, au amekaidi kuwasilisha Ushuru wa Mazao ya kilimo aliyokusanya kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hizi;

(c) Ameshindwa kuleta taarifa zozote ambazo zinahitajika kuthibitisha makusanyo yake ya ushuru unaohitajika kwa Halmashauri;

(d) Atamshawishi mtu yeyote asilipe au atamzuia mkusanya ushuru yeyote kufanya kazi yake;

(e) Ameshindwa kuwasilisha ritani, taarifa, kabrasha, au maelezo yoyote yanayohitajika chini ya Sheria Ndogo hizi;

(f) Ameshindwa kuweka vizuri kumbukumbu, vitabu, hesabu au maelezo yoyote yanayohitajika chini ya Sheria ndogo hizi;

(g) Ametengeneza, ametayarisha au ameidhinisha utengenezaji, utunzaji na utunzaji wa hesabu au nyaraka za uongo;

(h) Amemzuia Mkurugenzi au Afisa Muidhinishiwa kutekeleza kazi yake chini ya Sheria Ndogo hizi.

(i) Kosa lolote ambalo litaathiri utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

52. Kwamaba mtu yeyote atakiuka kifungu chochote kilichopo katika sheria ndogo hizi Atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria ndogo hizi na akithibitika kufanya kosa lolote kati ya makosa yaliyoorodheshwa katika sheria ndogo hii, atawajibika kulipa faini isiyopungua 200,000/= na isiyozidi Tshs. 900,000/= au kifungo cha miezi 12 au vyote adhabu ya kifungo na faini kwa pamoja.

53. Kwamba sheria ndogo hii inafuta sheria ndogo ya Halmashauri ya Butiama ya mwaka 2015 iliyotangazwa katika gazeti la serikali N0 265.

## JEDWALI LA KWANZA LA SHERIA NDOGO
## USHURU WA MAEGESHO WA MAGARI YANAYOINGIA STENDI

*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 7(1)*

| Na. | SAFU YA KWANZA: | SAFU YA PLI: kiasi cha ada |
|---|---|---|
| 1. | Gari linalobeba abiria 66 au zaidi | 10,000/= kwa siku |
| 2. | Gari linalobeba abiria 45-65 | 5,000/= kwa siku |
| 3. | Gari linalobeba abiria 30-44 | 4,000/= kwa siku |
| 4. | Gari linalobeba abiria 18-29 | 25,00/=kwa siku |
| 5. | Gari linalobeba abiria 6-17 | 2000/=kwa siku |
| 6. | Gari linalobeba abiria 1-5 | 1000/=kwa siku |
| 3. | Ushuru wa chombo cha chenye mzigo stendi | 2,000/= kwa siku |
| 4. | Ushuru wa kuingia stendi kwa mtu asiyekuwa na tiketi | 200/= siku |
| 5 | Ushuru wa gari binafsi zinazoingia stendi | 1,000/=siku |

## JEDWALI LA PILI LA SHERIA NDOGO

## USHURU WA MAZAO YA MCHANGANYIKO NA MAZAO YA BUSTANI

*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 8(1),9(1),9(3),10(1)*

| Na. | SAFU YA KWANZA: aina ya mazao | SAFU YA PLI: kiasi cha ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Mahindi | 2,000/= kwa gunia moja |
| 2. | Maharage | 2,000/= kwa gunia moja |
| 3. | Mtama | 2,000/= kwa gunia moja |
| 4. | Alizeti | 2,000/=kwa gunia moja |
| 5. | Udaga | 2,000/= kwa gunia moja |
| 6. | Viazi | 2,000/ kwa gunia moja isiyo rumbeza |
| 7. | Mpunga | 2000/= kwa gunia moja |
| 8. | Dengu | 2,000/= kwa gunia moja |
| 9. | Mazao Ya Bustani | 1000/= kwa tenga |
| 10. | Mazao mengine | 2000/= kwa gunia |
| 11. | Kibali cha kusafirisha mazao | 10,000/= kwa tani |
| 12. | Kibali cha kutumia skimu ya umwagiliaji | 50,000/= kwa mwaka |
| 13. | Ada ya utunzaji wa skimu ya umwagiliaji | 40,000/= kwa mwaka |
| | | |

## JEDWALI LA TATU LA SHERIA NDOGO
## USHURU WA MADINI UJENZI NA DHAHABU

*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 11(1),12(1),13(1),14(1),15(1),16(1),17(1),18(1),19*

| Na. | SAFU YA KWANZA: | SAFU YA PLI: kiasi cha ada |
|---|---|---|
| 1. | Kokoto | 3,000/= /trip |
| 2. | Mchanga | 3,000/= trip |
| 3. | Mawe | 3,000/= kwa trip |
| 4. | Moramu/Kifusi | 3,000/= kwa trip |
| 5. | Kiroba cha mawe ya dhahabu | 1,000/= kwa kiroba kimoja |
| 6. | Makinikia | 600,000/kwa senga |

| | | |
|---|---|---|
| 7. | Ushuru wa karasha | 15,000/=kwa mwezi |
| 8 | Ushuru wa madini pemba | 2,000/= kwa kiroba |
| 9 | Ushuru mwalo | 10,000/= kwa mwezi |
| 10 | Ushuru wa plant | 500,000/= kwa mwaka |
| 11 | Ushuru wa Bajaji yenye mchanga , mawe na kokoto | 1000/= kwa tripu |

## JEDWALI LA NNE LA SHERIA NDOGO
## USHURU WA MATANGAZO YA BIASHARA KWA NJIA YA SAUTI NA USHURU WA MOBILE SHO

*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 20(1),(2)(3)na 21*

| Na. | SAFU YA KWANZA: | SAFU YA PLI: kiasi cha ada |
|---|---|---|
| 1. | Matangazo ya biashara kwa njia ya Sauti | 50,000/= kwa siku |
| 2. | Mobile shop/kuweka kontena la biashara | 30,000/= kwa mwaka |

## JEDWALI LA TANO LA SHERIA NDOGO
## USHURU WASHUGHULIZA UTAMADUNI

*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 29(1)(2)(3),30,31(a)(b)(c)*

| Na. | SAFU YA KWANZA: | SAFU YA PLI: kiasi cha ada |
|---|---|---|
| 1. | Kibali cha sherehe | 20,000/= kwa siku atakazofanya sherehe |
| 2. | Wauza dawa za kienyeji mnadani au gulioni | 300/=kwa siku |
| 3. | Kibali cha kuendesha utafiti wa masuala ya kale | Raia tsh 50,000/=Asiye raia usd 70 |

## JEDWALI LA SITA LA SHERIA NDOGO
## USHURU WA UKAGUZI WA NYAMA

*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya ,23(1),24(1) 26,na 25*

| Na. | SAFU YA KWANZA: | SAFU YA PLI: kiasi cha ada |
|---|---|---|
| 1. | Ukaguzi wa nyama ya Ngombe | 5,000/= kwa @1 |
| 2. | Ukaguzi wa Nyama ya Mbuzi | 2,500/= kwa @1 |
| 3. | Ukaguzi wa nyama ya Kondoo | 2,500/=kwa@1 |
| 4. | Ukaguzi wa Nyama ya Nguruwe | 3,000/=kwa@1 |
| 5 | Ushuru wa kulaza ngombe machinjioni | 2,000/= kwa@1 |
| 6 | Ushuru wa kulaza kondoo manjioni | 1000/=kwa@1 |
| 7 | Ushuru wa kaulaza mbuzi machinjioni | 1000/=kwa@1 |
| 8 | Ushuru wa machinjio ya ngombe | 2000/= kwa@1 |
| 9 | Ushuru wa machinjio ya mbuzi | 1000/=kwa@1 |
| 10 | Ushuru wa machinjio ya kondoo | 1000/=kwa@1 |

## JEDWALI LA SABA LA SHERIA NDOGO
## ADA YA USOMAJI WA NYARAKA

*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 28(1)(2)(3)(4)(5)(6)*

| Na. | SAFU YA KWANZA: | SAFU YA PLI: kiasi cha ada |
|---|---|---|
| 1. | Kusoma nyaraka na kutumia maktaba ya Halmashauri | 5,000/= kwa siku |
| 2 | Kurudufisha nyaraka | 20,000/= kutegemea na nyaraka husika |

| | | |
|---|---|---|
| 3. | Kutumia maktaba ya Halmashauri | 5,000/= kwa siku |

**JEDWALI**

**USHURU WA MAZAO YA MIFUGO: USHURU WA MAZIWA, NGOZI NA VINAVYOHUSIANA NA MIFUGO**

*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo* ya *27 (1)(2)(3)(4)*

**Jedwali la Tatu:**

| Na. | SAFU YA KWANZA: aina ya mazaoya mfugo | SAFU YA PILI: kiasi cha ada |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa maziwa, | Tsh 50/= kwa lita moja |
| 2 | Ushuru wa ngozi | 5% ya bei ya kununulia mazao ya mifugo kutoka wa mfugaji anayezalisha mazao ya mifugo |

**JEDWALI**

**USHURU WA MAZAO YA MISITU**

*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya ,32(1)(2)(3)(4)(5)(6),33(1)(2)na 34(a)(b)(c)*

| Na. | SAFU YA KWANZA: | SAFU YA PLI: kiasi cha ada |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa mkaa gunia moja | 2,000/= |
| 2. | Ushuru wa mbao wanazovuna kila ubao | 1,000/= |
| 3. | Ushuru wa Asali kwa kg 1 | 1,000/= |
| | Kuni zilizopakiliwa ndani ya gari tani 1-3 | 20,000/= |
| 4. | Kuni zilizopakiliwa ndani ya gari tani 4-7 | 50,000/= |
| 5 | Kuni zilizopakiliwa ndani ya gari tani 7 au zaid | 100,000/= |
| 6. | Ushuru wa mirunda | 500/= kwakila mmoja |
| 7. | Kibali cha kuvuna mti | 1,000/= kwa kila mti |
| 8. | Ushuru wa Magogo yenye ujazo wa tani 1 | 15000/= |
| 9. | Kuni zilizopakiwa ndani Bajaji | 10,000/= |

**JEDWALI LA KUMI LA SHERIA NDOGO**

**USHURU WA BIASHARA SOKONI**

*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 35(1)(2)(3)*

| Na. | SAFU YA KWANZA: | SAFU YA PLI: kiasi cha ada |
|---|---|---|
| 1. | Biashara ya nguo za mitumba | 1,000/= kwa siku |
| 2. | Biashara ya nguo za madukani | 1,000/= kwa siku |
| 3. | Biashara ya viatu vya mtumba | 1,000/= kwa siku |
| | Michezo mbalimbali katika soko | 5,000/=kwa siku |
| 4. | Biashara za urembo | 1,000/= kwa siku |
| 5. | Biashara ya vyombo vya ndani | 1,000/=Kwa siku |
| 6. | Kibali cha kuweka kontena la biashara | 50,000/=kwa siku |
| 7. | Kibali cha kuweka kiosk/magazeti | 5,00/= kwa siku |
| 8. | Ushuru wa kuuza mazao katika masoko minada na magulio kwa wafanyabiashara wa mazao ya kilimo na mboga mboga | 1,000/= kwa mazao ya nafaka na 5,00/= kwa mazao ya bustani |
| 9. | Ushuru wa kizimba sokoni | 1,000/= kwa siku |
| 10 | Ushuru wa vileo | 4,000/= kwa siku |

| | | |
|---|---|---|
| 11 | Ushuru wa jiko | 1,000/= kwa siku |

**JEDWALI LA KUMI NA MOJA LA SHERIA NDOGO**
**USHURU MAEGESHO KATIKA MAENEO YA HALMASHAURI**
*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 36(1)(2)*

| Na. | SAFU YA KWANZA: | SAFU YA PLI: kiasi cha ada |
|---|---|---|
| 1. | Pikipiki | 2,00/= kwa siku |
| 2. | Bajaji | 5,00/= kwa siku |
| 3. | Gari lolote la mtu binafsi | 1,000/= kwa siku |
| 4. | Magari ya mizigo bila mizigo | 2,000/=kwa siku |
| 5. | Magari ya mizigo yenye mizigo | 3,000/= kwa siku |
| | | |

**JEDWALI LA KUMI NA MBILI LA SHERIA NDOGO**
**USHURU WA KULAZA MAGARI**
*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 37(1)(2)*

| Na. | SAFU YA KWANZA: | SAFU YA PLI: kiasi cha ada |
|---|---|---|
| 1. | Magari madogo ya watu binafsi | 1,000/= kwa usiku mmoja |
| 2. | Magari makubwa ya abiria na mizigo | 3,000/= kwa usiku mmoja |
| 3. | Mashine au mitambo ya ujenzi wa barabara au visima | 5,000/= kwa usiku mmoja |

**JEDWALI LA KUMI NA TATU LA SHERIA NDOGO**
**USHURU WA HUDUMA**
*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 38(1)(2)(3)(4)*

| Na. | SAFU YA KWANZA: | SAFU YA PLI: kiasi cha ada |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa Huduma kwa makampuni yanayofanya kazi katika Halmashauri | 0.3 asilimia |
| 2. | Tozo za kukodisha ukumbi wa Halmashauri | 100,000 |
| 3. | Tozo za kukodisha vyombo vya matangazo vya Halmashauri | 50,000 |

**JEDWALI LA KUMI NA TATU LA SHERIA NDOGO**
**USHURU WA HUDUMA**
*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 39(1)(2)(3)(4)*

| Na. | SAFU YA KWANZA: | SAFU YA PLI: kiasi cha ada |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa maliwato | 3,00/= kwa anayetumia |
| 2. | Ushuru wa kuoga | 500/= kwa siku |

**JEDWALI LA KUMI NA TANO LA SHERIA NDOGO**
**USHURU WA MAZAO YATOKANAYO NA SHUGHULI ZA UVUVI**
*Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 36 na 37*

| Na. | SAFU YA KWANZA: aina ya samaki | SAFU YA PILI: kiasi cha ada |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa samaki wakavu mnadani/gulioni | 2,000/kwa siku. |

| | | |
|---|---|---|
| 2. | Ushuru wa samaki wabichi mnadani/gulioni | 3,000/= kwa siku |
| 3. | Ushuru wa sangara | 2,00/kg |
| 4. | Ushuru wa sato | 2,00/kg |
| 5. | Leseni ya ukusanyaji wa samaki na mazao ya samaki | Shilingi 14,500/= |
| 6. | Ushuru wa vigugu | 5,00/kg |
| 7. | Ushuru wa dagaa | 150/kg |
| 8. | Ushuru wa kambale | 2,00/kg |
| 9. | Ushuru wa kamongo | 2,00/kg |
| 10. | Ushuru wa mabondo | 5,000/kg |
| 12. | Ushuru wa kugawa/maegesho | 3,000 /= kwa mwezi |
| 13. | Ushuru wa samaki wengineo | 1,50 /kg |
| 14. | Ushuru wa Furu | 1,50/kg |
| 15. | Kibali ca kusafirisa mazao ya samaki | 10,000/= kwa siku |

## JEDWALI LA KUMINA SITA SHERIA NDOGO
## USHURU WA KUMBI ZA HALMASHAURI

***Limetengenezwa chini ya sheria ndogo ya 22(a)(b)(c)(d)***

| Na. | SAFU YA KWANZA: | SAFU YA PILI: kiasi cha ada |
|---|---|---|
| 1. | Kwa taasisi inayohusisha wataalum wa Halmashauri | 100,000/= |
| 2. | Kwa taasisi isiyohusisha wataalum wa Halmashauri | 300,000/= |

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Butiama imegongwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa Azimio lililopitishwa na Mkutano wa Baraza la Halmashauri ulioitishwa tarehe ……. Mwezi wa ………………. Mwaka …………………….. na kushuhudiwa na:-

…………………………………………………….

Aziza J.Baruti

**MKURUGENZI**

**HALMASHAURI YA WILAYA**

**BUTIAMA**

…………………………………………………

PETER WANZAGI NYERERE

**MWENYEKITI**

**HALMASHAURI YA WILAYA**

**BUTIAMA**

**NAKUBALI**

……………………………………………………..

**Mohamed Mchengerwa (Mb)**

**OR- TAMISEMI –DODOMA**

LEO TAREHE ………………… MWEZI ……………..2025